

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA CHEMBA  
(Barua zote zielekezwe kwa Mkurugenzi Mtendaji  
Wilaya)

Unapojibu tafadhali taja;

Kumb.Na. CDC/A.60/3 VOL II /129

22/11/2023

Afisa Mtendaji wa Kijiji

Kijiji cha .....

S.L.P 830

CHEMBA

**YAH: MWALIKO WA MAFUNZO YA UJASIRIAMALI KWA WANAVIKUNDI NA  
WAJASIRMALI**

Husika na kichwa cha habari tajwa hapo juu.

Halmashauri ya Wilaya ya Chemba kwa kushirikiana na Taasisi isiyo ya Kiserikali ya **Star Entrepreneur General** kutoka Mkoani Morogoro ambayo inatambuliwa na **Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC)**, wataendesha Mafunzo ya Ujasiriamali kwa wanavikundi na wajasirimali. Mafunzo hayo yanatarajia kufanyika kuanzia siku ya **Jumatatu tarehe 27 Novemba 2023 mpaka Ijumaa tarehe 01 Desemba 2023** kuanzia saa 2:00 asubuhi mpaka saa 8:00 mchana katika **Ukumbi wa Abuu Shine Chemba**.

Lengo la Mafunzo haya ni kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kuongeza thamani ya mazao ya kusindika na kujipatia kipato. **Walengwa ni wananchi wote wanaofanya shughuli zao binafsi (wajasiriamali na wanaotoka kujifunza ujasiriamali) au waliopo kwenye vikundi vya ujasiriamali.**

**Mafunzo hayo yataendeshwa bure**, isipokuwa mshiriki **atajigharamia chakula, nauli na malazi** kwa wale wanaotoka nje na Kata ya Chemba

**Mada zitakazowezeshwa ni**

1. Utenegenezaji wa Biscut, Karanga za Mayai, na Tambi,
2. Uaandaaji wa lishe Bora,
3. Utengenezaji wa Batiki na Sabuni za Miche na Maji
4. Usimamizi wa Biashara,
5. Utafutaji wa Masoko,
6. Ufugaji wa Kuku.

**Washiriki watafundishwa kwa vitendo Utengenezaji wa Batiki na Sabuni za Miche.**

Kwa barua hii, unaagizwa kuwatangazia na kuwaalika wananchi, wajasirimali na wanavikundi waliopo katika eneo lako ili kuweza kupata fursa ya mafunzo haya.

Nakutakia utekelezaji mwema.



Rose Kitundu

Kny:- Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri (W)

**CHEMBA**

K.N.Y. MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
CHEMBA

**NAKALA**

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri (W)

– Kwa taarifa